Seed Savers Network
Kenya

Wafugaji wa Maasai na kalenjin kwenye eneo la bonde la Ufa Kenya wamehusika katika vita vya kusimamisha ubinafsishaji wa nyasi ambayo walipanda na kuwalisha mifugo yao kwa karne nyingi,. Ikiwa haki ya ubinafsishaji wa mimea itakubalika, jamii hawatakuwa na uwezo wa kuzalisha au kufanya biashara bila ruhusa na malipo ya mrabaha kwa kampuni za binafsi.

Rabsha hii yote huonyesha jinsi sheria na kanuni ambazo hutunza idara ya mbegu zimeundwa kufaidi makampuni ya watu katika migongano ya moja kwa moja na haki za wakulima na jamuiya za kiasili. kwa kesi la nyasi ya Buffel, anayetafuta haki ya kumiliki ya nkibinafsi Murray Roberts ametumia mlango wa ubinafsishaji wa mbegu ulioundwa na Kenya mwaka wa 2012 katika mkataba wa sheria la mbegu katika msingi wa UPOV 1991.

Hali hii inatuonyesha mifano jinsi wanaozalisha mimea hupuuza wakulima wanaozalisha vyakulaya , na kwa nini bara zima la Africa lazima likatae kabisa ubinaafsishaji wa viumbe hai.

Pendekezo

1. “Nyasi ni ya milima na kwa hivyo mbegu yake na ukulima kwa jumla hupasa kuwa ya kila mmoja na isiwe ya ubinafsi. Mzee Erige katika Kaunti ya Baringo Kenya anukuu akizungumza akitetea nyasi ya buffel ambayo kwa sababu ya sheria za UPOV sasa inatishia kubinafsishwa. https://grain.org/e/xxx.
2. Nyasi ya Buffel ni muhimu kwa wafugaji wa Kenya- inaweza tumika kama lishe kwa mifugo,kuezeka paa na mengine mengi. Lakini maamuzi ya mtu binafsi kuibinafsisha inatia hofu ya kuinyakua na kupokonya wanajamii. Hii inaashiria jinsi jambo hili la ubinafsishaji wa viumbe hai linafaa kukataliwa kabisa katika bara hili https://grain.org/e/xxx.

3. Maamuzi ya Kenya kutumia misingi ya sheria la mbegu ya 2012 kwa UPOV 1991 huashiria upungufu mkubwa kwa kanuni zilizoundwa kufaidi watu binafsi na makampuni chache kwa dhamana ya haki. Kinachofanyika kwa jamii ya Wamaasai kwa Nyasi ya buffel ni mfano maalum: https://grain.org/e/xxx.

WACHANA NA NYASI YETU! WAFUGAJI WA KENYA WANAPINGA UBINAFSISHAJI WA BIOANUWAI ZAO

Shirika La Grain Na Seed Savers Network Kenya.

Wafugaji sanasana hupuuzwa kama wamiliki wa bioanuwai zao Katika Bara la Africa. Licha ya changamoto kadhaa wanazopitia kama vile kuwekewa vizuizi

kwa njia za uhamiaji, vita na ukosaji wa shule na huduma za afya- mifumo ya chakula wanayoongoza imebaki kuwa yenye ustahimilivu Zaidi katika maeneo kavu wanayoishi isipokuwa mashamba na nyasi wanayo fuga wanyama wao ibinafsishwe.

Jambo hatari la taswira kama hili linatishia wafugaji wa jamii ya waKalenjin na wamaasai katika Bonde la ufa nchini Kenya. Wamaasai na Wakalenjin kwa sasa wanahusika kwenye vita vya kusimamisha ubinafsishaji wa nyasi ya buffel ambayo jamii imelisha mifugo yao tangu nyakati za kale. Jambo hili ni mfano wa jinsi haki ya wafugaji wa mimea (PBRs) ubinafsishaji katika mimea inaweza kudhoofisha wakulima wa vyakula katika bra la kiafrika na kwa sababu hii bara nzima lafaa kukataa kabisa umiliki wa viumbe hai.

Umuhimu wa nyasi ya buffel kwa wafugaji wa kenya

Geoffrey Letakaan wa umri wa miaka 63 ni mzee katika jamii ya kalejin wafugaji wanaoishi katika Kaunti ya Baringo Kenya. “Nyasi hiyo imekuwa tangu enzi za babu za babu zetu” anukuu Letakaan. Nyasi hii inadhamana sana, ukiwalisha Ng’ombe hunona katika mda wa miezi mitatu na pia inatumika kwa kuezeka nyumba na kutengenewa mifugo kama lishe wakati wa ukame. Zamani, wazee walikua wakisema”nangrongong” kumaanisha nyasi ya buffel hiyo iko milimani eneo la arabal na mukutani na kila mtu anapaswa kupanda nyasi hiyo.

Maoni yake yanasimamaia wengi katika kaunti ya Baringo, eneo la nyika katika bonde la ufa ya Kenya. Jamii ya ilchamus ama wamaasai na kalejini ni wafugaji wanaotegemea ngombe na mifugo wengine.

Wafugaji wa Baringo hujulikana kwa upandaji wa nyasi ya foxtail inayojulikana kama buffel barani Africa. Tangu nyakati za kale, wanajamii wamelisha mifugo yao kwa nyasi ya buffel ambalo jina lake la kisayansi ni Cenchrus ciliaris. Wenyeji huita nyasi hiyo lhoggor ainyok baina ya ilchamus na lhomer kwa watugen, kabila ndogo ndani ya kabila ya kalenjin. Wanatumia nyasi hiyo kama muda mrefu na malisho ya kudumu maana imezoea aina ya udongo,

humea haraka ata kwa mvua ndogo na hujulikana kama nyasi pekee inayostahimili ukame.

Katika eneo la Baringo na sehemu zingine za Kenya ambazo ni kame nyasi ya buffel ni muhimu na ni hodari katika matumizi yake kando na kutumia kuziuza na kuweka kama lishe ya mifugo nyakati za ukame, ikiwa na protini ya hali ya juu ya asilimia kumi na mbili , Nyasi hunenepesha mifugo kwa haraka, Baadi ya jamii hununua mifugo waliodhoofika kwa bei ya chini kisha kuwanenepesha kwa nyasi ya buffel na baadaye huuza baada ya miezi mitatu .Pia mbegu hizi huuzwa kwa gharama ya juu shilingi300 (US$ 3) hadi shilingi 750 (7.5 US$) kwa kilo moja.

Wanawake huwajibika kuwalisha mifugo kwa jamii ya wafugaji wakati wanaume hushugulikia lishe kwa hivyo wanawake hutegemea nyasi ya buffel zilizofungwa kwa mafungu na kuhifadhiwa hasa kuwalisha ndama wachanga wakati wa kiangazi.

‘’naenda tu kwenye ghala na kutwaa nyasi zilizifungwa kisha nawalisha mbuzi na ndama” asema Sahlline Parkolwo mwenye umri wa miaka ishirina na tisa. Alibainisha kwamba wakati ndama na watoto wamelishwa vizuri hawaitaji kunyonya sana kwa hivyo maziwa mengi yanapatikana kwa matumizi ya famillia, hivyo kwa watoto na wazee wakongwe kwa hivyo inaathiri vyema kwa uhuru wa vyakula, kwa kuongezea, wanaume wanajenga nyumba ya kiasili, wanawake hupewa jukumu la kutafuta nyazi.

Nyasi ya buffel ni nzuri kwa kuezeka nyumba kwa sababu ni imara na pia wanawake nao wanaweza kuuza mbegu za nyasi hii ili wapate mapato itakayotumika kwa matumizi ya kibinafsi na ya familia .

MURRAY ROBERTS

kwa miongo michache iliyopita, mwanaume kwa jina Murray Roberts, anayejulikana kwa jamii ya wakalejin na ilchamus kama “Omari” ameongoza juhudi za mabadiliko ya usimamizi wa nyasi ya Buffel- kutoka kwa mfumo wa

ardhi ya jumuiya kwenda kwa umiliki wa mashamba na jamii ya wafugaji hadi umiliki wa ubinafsi na kilimo cha kina.

1. kalenjin ni jamii hasili ambao wanaishi katika bonde la ufa

2.AFSA (2018) JAMII YA WAFUGAJI: Chakula kwa uwingi: inapatikana kwa wafuti https://afsafrica.org/case-studies-pastoralism/

3. wanajamii hawakuweza kutamka jina lake vizuri hivyo basi akaitwa " Omari"

Roberts ni mkenya ambaye ni baadhi ya walowezi wazungu ambao walipata shamba katika kaunti ya Baringo wakati wa ukoloni wa Uingereza na kuanzisha biashara lenye faida kubwa sana ya familia eneo la uhifadhi wa mbegu na utalii.

Mwaka wa 1982, Roberts alianzisha shirika la uhifadhi " Rehabilitation on Arid Environments (RAE) Trust" , kubadilisha nchi kavu iliyoharibiwa ili iwe nyanda za malisho na kufaidi jamii na mazingira. RAE imekuwa ikijaribu kufanya hivyo kwa kuandikisha jamii ili wawe wakulima wa nyasi ya Buffel na kuwashawishi jamii kuwapa viwanja hili wafanye ukulima, Roberts kwa maneno yake mwenyewe amenukuu " Tulianza mwaka wa 1982 kwa sababu ya mfadhili, Tuliruhusiwa tu kushirikisha jamii kwa hivyo tulikuwa na viwanja vingi vya jamii, wakati mfadhili alipoondoka, tukaenda kwa mtu binafsi, hapo ndipo tulipata utofauti mkubwa kwa sababu tulianza kupanda kwa mashamba ambayo mahindi yamepandwa, tulianza kupanda nyasi kwa mashamba yao. Bibi yangu ndiye alikuja na wazo hili, la kupanda ardhi ya kibinafsi amabalo wazo hili liishangoa nanga. Ukulima wa malisho umeunda kiwanda kaunti ya Baringo. kiwanda hicho kinaendelea na hata hainitegemei kwa sasa hivi kwamba niwe nisiwe kitaendelea kwasababu hakinitegemei kwa sasa. mashamba ya pamoja ya jamii yanaweza isha nikitoka kwasababu hakuna mtu kwa jamii hizi atakaye angalia mambo ya jamii, wanataka tu kula."

Wenyeji wanasema juhudi za RAE zimebadilisha uhusiano wao na nyasi ya buffel " Nyasi ya Buffel zimekuwa hapa kwa miongo mingi, jambo tu moja amabayo jamii haikujua ni uwezo wa kibiashara", mwanajmi George Letakan asema.

Leo hii wanajamii weingi huzalisha na kuuza mbegu ya nyasi ya Buffel, wengine wanauza kupitia RAE na weingine wanauza kupitia Kerio Valley Development

Authority (KVDA) ambayo ni wakala wa serkiali yamkoa, umoja wa wana jamii, Jackson Lekombe , ambaye amechagua kutouza mbegu ya nyasi kwa RAE anasema anauza moja kwa moja kwa KVDA kwa pamoja kwa kupitia kikundi cha wakulima cha Noonseiya chenye wanachama 25 ambao hujihusisha na ukuzaji na uhifadhi wa mbegu.

Unyakuzi Wa Mbegu

Juhudi za Roberts za kubinafsisha mbegu ya nyasi ya Buffel haikuishia kwa kukwepa jamii na kushirikisha watu binafsi.Mwaka wa 2012, Robert alianza mipango ya kuzalisha nyasi hii.Alituma ombi la kupata cheti cha kubinafsisha na akapewa cheti cha mda mfupi cha kumruhusu kuzalisha nyasi hii.kulingana na shirika na afya ya mimea nchini (KEPHIS) nyasi anayedai Robert inaitwa Baringo 1.

Alipopewa cheti hichi, Baringo 1 mimea huu ulijumuishwa kwa oroda ya aina za tofauti ya mbegu za kitaifa za Kenya, inamaana kwamba mbegu yake haiwezi ikauzwa bila idhini yake. Mwaka wa 2014, Roberts alichukua hatua zaidi na kuomba haki ya uzalishaji wa mimea (plant breeders' Right) kwa Baringo 1, kwa lengo la kutwaa umiliki kamili kwa gharama ya haki ya wakulima, Roberts alikusudia kuandikisha aina tano zaidi kwa idara ya kudhibiti mbegu

4. kipengele cha historia hii ya familia kimeelezwa kwenye tovuti kama kama kampuni inayoendeshwa na Murray Roberts http://robertssafaris.com/our/history na http://www.raetrust.org/

6. " sehemu ya pili uharibifu na upunguzaji wa ardhi Barani Afrika , tathmini, kupunguza na kurekebisha" imehaririwa na Pandi Zdruli, Marcello Pagliai, Selim Kapur, Angel Faz Cano Springer, Science and Business Media, 2010 p. 117

7. waliohojiwa na Seed Savers Network, Machi 2020.

8. Sehemu ya sheria ya aina ya mbegu na mimea ya Kenya, 2010 iliweka masharti ya kutoa haki ya wazalishaji wa mimea.

Chini ya sheria ya Kenya mbegu aina za mimea 2012 ambayo imejikita katika utoaji wa umoja kwa ajili ya ulinzi wa mkataba mpya wa aina za mimea wa laai (UPOV 1991) uzalishaji wa mbegu yeyote, iwe ni ya umma au binafsi, wenyeji au wageni wanawezakuomba na kupata haki za ubinafsi juu ya aina mpya yammea ambao wamegundua au kuzalisha, hii inaweza kwa bahati mbaya kujumuisha aina mbalimbali za mbegu za wakulima na hapa ndipo mzozo unatokea kwa nyasi za RAE.

“Kwa wakulima wengi wa mifugo, ni kujaribu tu kudai umiliki wa bioanuwai zao, Erige, mkaazi wa Baringo anukuu.

Wakati ambapo jamii waligundua hila ya Roberts kuhusu ombi lake la kupata ubinafsishaji wa haki ya ukuzaji, wazee wa mtaa walikwea mmlimani na kukusanya sampuli ili kulinganisha na aina ya mbegu inayokuzwa na RAE, waligundua ya kwamba inafanana, kulingana na Erigr, “ Nyasi ni za mlima na kwa hivyo mbegu na ukulima wake inapaswa iwe ya kila mtu na haipaswi kubinafsishwa”.

Wamefarijiwa katika mtazamo huu na katiba ya Kenya iliyo fanyiwa marekebisho mwaka wa 2010 inayosema ya kwamba, jamii itafurahia umiliki wa mbegu za asili na aina za mimea, maumbile yao na sifa mbalimbali na maatumizi yao,kwa kuzingatia katiba, wakaazi wa Baringo wanapaswa kuwa na haki ya Kijamii kumiliki nyasi ya Buffel, hata hivyo, kifungu cha mimea na aina mbalimbali cha katiba, 2010 kinapinga na kumruhusu Robert kupata haki yake ya kibinafsi juu ya nyasi za buffel, matokeo yake kuna mgongano kati ya wafugaji na haki ya wakulima nchini Kenya.

Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Kerio (KVDA) pia inapingaa ombi la Roberts (PBR), mwaka wa 2016 KVDA ilimwandikia barua inayosema kuwa imekua ikifanya majaribio na kuuzalisha *cenchrus Ciliaris* tangu 2001 na nyasi ilikuwa imeingia majaribio ya kitaifa, ilisema kwamba RAE haikuweza kuzalisha aina iliyowasilishwa kwa sababu haikuwa na mpangilio ya uenezaji wa mimea, zaidi ya hayo KVDA ilisisitiza ya kwamba nyasi ya Buffel inafaa kumilikiwa na umma na maswala yao kuzingatiwa.

Shirika la Utafiti wa Kilimo na Mifugo la Kenya (KALRO) laeleza kuwa hali ya huzuni hii inamaana kwamba inazalisha bila kujamiiana kupitia mbegu. Mtu yeyote anayedai ametengeneza aina mpya yake anastahili kueleza hatua za uzalishaji aliyochukua hadi sasa .RAE imeshindwa kupeana mbinu zake, KALRO yasema nimuhimu kutambua. Nyasi hii pia hukuzwa kwa majimbo mengine kama Kitui, Marsabit, Mandera, Kilifi na Makueni, kwa mtazamo wa KALRO, kwa idadi ya *cenchrus Ciliaris, imegunduliwa* kwamba Baringo 1 ni kati ya ecotype tofauti kwa asilimia 99 ya wakati.

Mwaka wa 2016 , KEPHIS ilipanga mkutano na Roberts, Jamii, KVDA na KALRO kupata suluhu la kirafiki kwa mzozo huo, mashirika ya umma Kenya kama wizara ya Kilimo , Mifugo na Uvuvi ilipinga ombi la Murray (PBR) anasema aina mbegu mbalimbali zinazizingatiwa zilikuwa na manufaa ya kuwa aina asili na maarifa ya kawaida, lakini Murry hakutikisika mara kwa mara alifuruga mkutano kwa kusimama nakurushia lawama Jamii kwa kutwaa “Mbegu yake” , Murray alidai ya kwamba ni yeye tu ndiye mwenye haki ya kukuza mbegu ya nyasi ya buffel, kwa hivyo Jamii, KVDA na mzalishaji mwingine wa mbeguj hii wanavunja Sheria.

10. kifungu kidogo cha Katiba cha 2 kinasema kwambaa mwombaji haki ya uzalishaji wa mimea awe mtu aliyezalisha au kugundua aina ya mmea husika au mrithi wake kwa cheo , na Masharti ya sehemu ya 1 ya jedwali la nne yatakuwa na athari kuhusu vipaumbele kati ya watu wawili au zaidi ambao wamejitegemea kuzaliana au kugundua aina ya mmea.

Sheria ya Kenya. Katiba ya Kenya kifungu cha 3 (b). inapatikana kwa wavuti http://kenyalaw/kl/index.php? id=398

11 kulingana na hati zilizoonekana za waandishi

12. kulingana na KALRO.

13. Mahojiano na Seed Savers Network, Machi, 2022

Nini Kiko Hatarini?

Hatari katika mzozo huu ni haki ya wakenya wa wakulima kuokoa mbegu zao, kubadilishana kuuza mbegu za nyasi za buffel, ikiwa PBR itakubaliwa hatwataweza kuzalisha au kufanya biashara ya mbegu bila ruhusa ya Roberts . Hii itaathiri moja kwa moja na hasi ya wananchi na viongozi wa jamii hawaamini kwamba Roberts alizalisha mbegu hii . Wanapinga rasmi uhalali wa uwasilishaji wake kwa orodha ya kitaifa na mamlaka ya haki za uzalishaji wa mimea.

Ni muhimu kufahamu ya kwamba RAE haiko peke yake kwa kutafuta umiliki ya nyasi ya Buffel.

KALRO na KVDA zote ni taasisi ambazo zinatafuta umiliki wa kipekee wa ujio wake, Vita kati yao inachochewa na ukweli ya kwamba RAE imewazidi ujanja kwa kuandikisha nyasi hii. “KALRO inauwezo wa kutenga wengine, Tarizo si taasisi yoyote ila Sheria ya Mbegu, kwa UPOV Laai ambapo Jamii inaendele kuangaika, viumbe hai wanaendelea kuteseka na haki za wakulima hailindwi “ Daniel Wanjama asema ambaye ni Mkurugenzi wa Seed Savers Network, Kenya.

Jamii za Baringo hawana uhakika kuwa Ombi la Murray la PBR bado linasubiri kuidhinishwa. kwa KVDA imezindua hatua za kisheria kukomesha hilo katika jaribio hatua za kisheria kukomesha hilo katika jaribio bila mafanikio , wakati huo huo, Murray Roberts na RAE inaendelea kukuzaa mbegu na kuuza bila kuzingatia kesi hivyo, hatishii tena jamii kuhusu “ “Kupanda mbegu yake” kama alivyozoea.

Kwa sasa wanajamii wa Baringo wameamua kuendele kupanda nyasi je Buffel na kupuuza Madai ya Murray kuhusu mbegu kwenye safari hii wakulima wameungwa mkono na wizara ya kilimo ambao wamekuja wazi na kusema haki ya ukuzaji ya Baringo 1 haipaswi kupeanwa. Hata hivyo hii ni “ Juudi bure na si chochote zaidi ya zoezi la mahusiano ya umma kwani haki ya wakulima ilikuwa tayari wamenyanganywa wakati aina ya Baringo 1 iliposajiliwa katikaka orodha ya aina ya mimea ya kitaifa ” , Dominick kutoka Seed savers Network Kenya asema.

Twasema Hapana kwa RAE, hapana kwa KVDA, hapana kwa umiliki wowote mbegu.

Mzozo huu wote inaonyesha jinzi sheria na kanuni zinatawala sekta ya mbegu na zimetungwa kufaidi kampuni ama mtu binafsi kinyume na haki ya wakulima na

jamii, kwa upande wa nyasi ya Buffel, Murray anatumia tu mlango wa kutumia ubinafsishaji ulioanzishwa na sheria ya Kenya ya mbegu na aina mbalimbali ya sharia 2012- kwa kuzingatia UPOV 1991.

Ilikuwa ni swala la muda kabla ya maslahi kama ya RAE kukumbatia ukiritimba wa kisheria ya kudai udhibiti wa upekee juu ya aina mbalimbali za mbegu. Kwa kawaida, ulinzi wa kweli wa uzalishajiwa mbegu na wakulima utakuja pale tu Kenya itakapokataa sheria ya mbegu kwa kuzingatia UPOVU. Jaribio la sasa ikiwa KVDA na mamlaka nyingine zaumma kumzuia Murray kuaachana na PBR . Ubinafsishaji wa mbegu, hata ikiwa mpango wa RAE kupata PBR itaaanguka, wafugaji wa Baringo bado watapoteza haki yao ya kutumia nyasi kuhifadhi na kuzalisha nyasi ya baringo iwe kutoka KVDA ama sekta nyingine. Jaribio lolote laa kulinda mimea ya Kenya na mimea ya aina mbalimbali lifanywe kupitia walinzi wake wa kweli: wafugaji, wakulima na jamii ambazo zimejitafutia riziki kwa kutumia mimmea hii kwa kizazi.

TABLE ONE MPANGILIO WA MATUKIO	
KIPINDI/MWAKA	MATUKIO
Mpaka 2010	Wafugaji wa kalenjin na Maasai wamekuwa wakilisha mifugo yao katika ntyanda zao
1982	Murray Roberts kupitia shirika lisilokuwa ya Kiserikali (NGO) RAE Trust ilianza hatua za kutumia nyasi ya Buffel nakuhusisha Jamii ya Baringo.
1991	Mkataba wa UPOV ulirekebishwa huko Geneva kwa Muundo wake wa Sasa.
2001	Murray Roberts alianzisha hatua ya kuzalisha nyasi ya buffel.
2010	Kenya ilipitisha katiba mpya ambayo inatambua haki za jamii wenyeji kwa mbegu zao na maarifa ya jadi yanayohusiana.
2012	RAE Trust ilipokea cheti cha ruzuku ya mwelekeo wa kinga kwenye aina ya nyasi ya Buffel, iliyotolewa na KEPHIS>

Disemba 2012	Sheria ya Kenya ya mbegu na aina za mimea (marekebisho) ya 2012 imepitishwa.
2014	Mzozo kati ya jamii za Baringo , RAE Trust na KVDA kuhusu ombi ya haki ya uzalishaji RAE.
2016	Kenya inajiungan a UPOVU 1991 na kufungwa kikamilifu mkataba huo.
2017	Serikali inachapishwa cheti cha mwisho cha RAE katiks soko la nyasi ya BAringo 1